

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA**
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)

MKOA WA TABORA
SIMU: 026-2604315/2606088
FAX: 026-2604835



OFISI YA MKURUGENZI
S. L. P. 174
TABORA – TANZANIA

Kmb. Na. LGA/124/2018/2019/W/63/05

15 FEBRUARI, 2019

**TANGAZO LA KUJENGA VIBANDA, KUENDESHA NA KUREJESHA
(BUILD OPERATE AND TRANSFER)**


Na LGA/124/2018/2019/W/63

Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora anawatangazia wafanyabiashara wote kuwa Manispaa ya Tabora inatarajia kujenga vibanda ishirini na tano (25) katika eneo la maegesho ya Taxi, stendi mpya ya mabasi ya Manispaa ya Tabora.

Ujenzi huu unashirikisha jamii/wafanyabiashara kwa makubaliano ya kujenga, kuendesha na baada ya mkataba atarejesha kibanda na kumilikiwa na Manispaa Masharti ya waombaji wa vibanda hivi ni kama ifuatavyo:

1. Mwombaji ni lazima awe mfanyabiashara na awe na uwezo wa kifedha ili ujenzi uanze kwa pamoja ili kurahisisha usimamizi.
2. Mwombaji atajenga kibanda kwa kutumia michoro itakayotolewa na ofisi ya mkurugenzi wa manispaa.
3. Mwombaji atajenga kibanda chini ya usimamizi wa mhandisi wa manispaa kwa kila hatua ya ujenzi kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika Serikalini.
4. Mwombaji atawasilisha gharama za ujenzi kulingana na michoro/ramani za kibanda ambazo zitotolewa baada ya kulipa ada ya zabuni.

5. Mwombaji atakayepata na kufanya ujenzi wa kibanda, uthamini wa kibanda utafanyika ili kujua gharama halisi za ujenzi ambayo itafanywa na ofisi ya mkurugenzi wa Manispaa kabla ya kuingia mkataba wa uendeshaji.
6. Baada ya kumaliza ujenzi na uthamini kufanyika muombaji hataruhusiwa kufanya biashara kabla ya kufika ofisi ya mkurugenzi kwa ajili ya kuingia makubaliano wa muda wa kuendesha kibanda ili kurejesha gharama zake.
7. Muombaji hataruhusiwa kuipangia ofisi ya mkurugenzi wa manispaa bei ya kibanda na awe tayari kukubaliana na bei zitakazopangwa kulingana na bei ya soko na awe tayari kulipa manispaa kiasi kitakachokubalika (%) kulipwa na kiasi kingine (%) ataachiwa mjengaji ili aweze kufidia gharama zake.
8. Muombaji atakayefanikiwa kupata mkataba hataruhusiwa kupangisha kipanda bila idhini ya ofisi ya mkurugenzi na kufanya hivyo atakuwa amekiuka masharti ya mkataba na atayanganywa.
9. Mwombaji atakayefanikiwa kupata hataruhusiwa kufunga kibanda au kukifanya stoo.
10. Mwombaji atakayefanikiwa kupata kibanda akiamua kufanya biashara ya chakula hataruhusiwa kupika ndani au karibu na kibanda ili kuepusha ajali ya moto.
11. Mwombaji asiwe na historia ya kudaiwa kodi na Manispaa.
12. Mwombaji awe tayari kukamilisha ujenzi katika kipindi cha mienzi mitatu (3) na kushindwa kufanya hivyo mwombaji atakuwa amepoteza haki yake na mkataba utavunjwa.
13. Watumishi wa umma wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Madiwani hawaruhusiwa kushiriki kwenye zabuni hii.
14. Mwombaji awe na leseni ya biashara na TIN.
15. Biashara za Mbao, Magogo, Mkaa na Pombe za kienyeji hazitaruhusiwa katika eneo hili.
16. Mwombaji aandike barua ya maombi na kuwasilisha ofisi ya *Katibu wa bodi ya zabuni Manispaa ya Tabora, S.L.P 174* kabla au ifikapo tarehe 21/02/2019 siku ya Alhamisi saa 4.30 asubuhi. Ufunguzi utafanyika saa 5.00 asubuhi katika ukumbi wa manispaa.
17. Ada ya zabuni hii ni Tsh.100, 000.00 ambazo zitalipwa ofisi ya mweka hazina wa manispaa.
18. Muombaji atakayewasilisha maombi nje ya muda uliopangwa atakuwa amepoteza sifa ya kuingizwa katika mchakato wa zabuni hii.


Bosco O. Ndunguru
MKURUGENZI MANISPAA
TABORA